Toleo 81 - Rabi' al-Awwal 1445 H / Oktoba 2023 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Ushawishi wenye Sumu wa Marekani na Athari Zake Mbaya

**HABARI NA MAONI**
Ni Uislamu Tu Ndio Wenye Suluhisho la Kweli kwa Usalama wa Chakula kwa Afrika

**HABARI NA MAONI**
Vladimir Putin Amechukua Mahali pa Karimov

**JIBU LA SWALI**
Mabalozi katika Uislamu



# Sa’ad bin Muadh, Mkuu wa Ansar (ra)…

# Ni nani Sa’ad wa Ummah Huu hivi leo?!

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Bilal al-Muhajir – Wilayah Pakistan**

Kuwataja watu wakubwa wa historia ya Uislamu, sio kama kutaja habari za kale zozote za “mashujaa” wa kihistoria. Tafauti baina ya historia ya Waislamu watukufu na “mashujaa” wa historia ni kuwa usomaji wa habari za Waislamu watukufu ni kwa sababu ya kufuata mifano yao. Tunafuata nyayo zao, na kuchukua mafunzo kutoka kwenye matendo yao ya kishujaa. Kumbuka kuwa hawakufanya hayo matendo ya kishujaa kwa sababu walikuwa “hekaya za zamani.” Bali walifanya hayo kwa sababu walifahamu Uislamu kuwa ni aqida na hukmu za Shariah. Walitekeleza hukmu hizi kwa ukamilifu, na hivyo walijitafautisha. Walikuwa miongoni mwa wenye ushupavu na ambao nususi za wahyi ziliwatukuza. Miongoni mwa mashujaa hao ni swahaba mtukufu, Sa’ad bin Muadh, mkuu wa Ansar (ra).

Yeye (ra) ni miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu (swt) amesema,

**وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ**

**“Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajir na Ansar, na waliowafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.”** [Surah At-Tauba 9:100]

Swahaba huyu mtukufu (ra) anastahiki heshima hii na hadhi hiyo, kwa tendo lililo bora. Ilikuwa ni tendo kubwa la kijasiri ambalo viongozi wa Kikureshi, Waarabu na viongozi wengine walikataa kufanya. Ni tendo kuu la Nusrah kwa Uislamu na Mtume wake (saw). Kwa hivi, watu wenye nguvu hivi leo lazima watambue kuwa dola ya Kiislamu ilisimamishwa mara baada ya Sa’ad kutoa Nusrah kwa Muhammad (saw). Lazima wafahamu kuwa hadhi ya yule anayesimamisha Uislamu hivi leo atakuwa kama yule aliyetoa Nusrah kwa Mtume (saw).

Cheo chake insha Allah, ni kama cheo cha Sa’ad bin Muadh (ra), ambapo kuhusiana naye Mtume (saw) amesema,

**اهْتَزَّ الْعَرْشُ لِمَوْتِ سَعْدِ بْنِ مُعَاذٍ “Arshi ilitetemeka kwa mauti ya Sa’ad bin Muadh.”** [al-Bukhari and Muslim]. Adh-Dhahabi (rh) amesema, **هذا متواتر أشهد بأن رسول الله صلى الله عليه وسلم قاله “Hii ni mutawaatir. Nashuhudia kuwa Mtume (saw) ni hakika amesema hilo.”** [al-‘Uluw li’l-‘Aliy al-Ghaffaar]. Adh-Dhahabi ameielezea hii kwa urefu katika kitabu chake al-Fawaa’id, kutoka kwa Abu Sa‘iid al-Khudri (ra) ambaye amesema, “Mtume (saw) amesema,

**اهْتَزَّ الْعَرْشُ لِمَوْتِ سَعْدِ بْنِ مُعَاذٍ ، مِنْ فَرَحِ الرَّبِّ عَزَّ وَجَلَّ “Arshi ilitetemeka kwa mauti ya Sa‘ad ibn Mu‘adh, kwa sababu ya furaha ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.”** Katika as-Sunnah ya ‘Abdullah ibn al-Imam Ahmad, imesemwa, عَنِ الْحَسَنِ قَالَ لَقَدِ اهْتَزَّ عَرْشُ الرَّحْمَنِ جَلَّ وَعَزَّ بِجِنَازَةِ سَعْدٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ فَفَسَّرَهُ الْحَسَنُ فَرَحًا بروحهُ “Imepokewa kwamba al-Hasan amesema, imetikisika Arshi ya Ar-Rahman Aliyetukuka kwa maziko ya Sa’ad ibn Muadh (ra). Al-Hassan amefasiri kuwa ni furaha kwa roho yake.”

Inampasa kila kamanda wa Kiislamu kusoma kuhusu Sa’ad (ra) na kuzingatia. Ni Sa’ad (ra) aliyesimama siku ya Badr, siku ya al-Furqan, na kumwambia Mtume (saw), لقد آمنا بك وصدقناك... وشهدنا أن ما جئت به هو الحق، وأعطيناك على ذلك عهودنا ومواثيقنا على السمع والطاعة لك، فامض يا رسول الله لما أردت فنحن معك، فوالذي بعثك بالحق لو استعرضت بنا البحر فخضته لخضناه معك ما تخلف منا رجل واحد، وما نكره أن تلقى بنا عدونا غداً، إنا لَصبرٌ في الحرب، صُدقٌ عند اللقاء، لعل الله يريك منا ما تقر له عينك، فسر على بركة الله “Tumekuamini na kukusadiki juu ya ulichokuja nacho kuwa ni haki, na juu ya hilo tumekupa ahadi na ithibati yetu juu ya kukusikiza na kukutii. Basi amua ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu; na sisi tupo pamoja nawe. Naapa kwa yule aliyekuleta kwa haki lau ukituamrisha kuchupa baharini nasi tutachupa pamoja nawe, na hatokuhalifu yeyote kati yetu. Hatutochukia kukutana na adui yetu kesho, sisi ni wenye Subira katika vita, wakweli katika mapambano. Mwenyezi Mungu akuonyeshe kutoka kwetu kile kitakachotuliza macho yako, basi na tutegemee baraka za Mwenyezi Mungu na usaidizi wake.”

Hili ndio jambo ambalo watu wenye Nguvu na Nusra kutoka kwa makamanda na maafisa kwenye jeshi la Waislamu lazima walitambue, kuhusu msimamo wa watu, katika kuamua majaliwa ya Ummah. Hii ni kuwa wanatumia maisha yao kama alivyokuwa Sa’ad, katika kumtii Mwenyezi Mungu (swt). Hakika, Sa’ad alifahamu kwa usahihi maisha ya dunia. Kwa hivyo, yeye (ra) alitekeleza jukumu la kutoa Nusrah kwa Uislamu na Mtume wake (saw) katika kusimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu juu ya ardhi. Kifo chake kilikuwa kama bwana harusi aliyepambwa kwenye bustani za Peponi. Huyu ndiye Sa’ad ambaye watu walimwambia Mtume (saw), ما حملنا يا رسول الله ميتاً أخفَّ علينا منه “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hatukuwahi kubeba maiti nyepesi kama hii”. Juu ya jambo hili Mtume (saw) akasema,

**مَا يَمْنَعُهُ أَنْ يَخِفَّ وَقَدْ هَبَطَ مِنَ المَلاَئِكَةِ كَذَا وَكَذَا، لَمْ يَهْبِطُوا قَطُّ قَبْلَ يَوْمِهِم، قَدْ حَمَلُوْهُ مَعَكُم**

***Endelea... UK 3***

**“Hakuna kilichofanya mwili wake kuwa mwepesi isipokuwa kuna Malaika kadha na kadha wameshuka na kumbeba pamoja nanyi ambao hawakuwahi kushuka kabla ya siku hiyo.”** [imenukuliwa kutoka Tabaqat, ya ibn Sa’ad.]

Huyo ndiye Sa’ad (ra) ambaye alipokufa Jibril (as) alikuja kwa Mtume (saw) na kusema, من هذا العبد الصالح الذي مات؟ فتحت له أبواب السماء وتحرك له العرش “Ni nani huyu mja mwema aliyekufa? Milango ya mbingu imefunguka na Arshi imetikisika kwa ajili yake.” Mtume (saw) akasema,

**هَذَا الْعَبْدُ الصَّالِحُ الَّذِي تَحَرَّكَ لَهُ الْعَرْشُ، وَفُتِحَتْ لَهُ أَبْوَابُ السَّمَاءِ، وَشَهِدَهُ سَبْعُونَ أَلْفاً مِنَ الْمَلَائِكَةِ لَمْ يَهْبِطُوا إِلَى الْأَرْضِ قَبْلَ ذَلِكَ، وَلَقَدْ ضُمَّ ضَمَّةً ثُمَّ أُفْرِجَ عَنْهُ**

**“Mja huyu mwema ambaye Arshi imetingishika kwa ajili yake na milango ya mbingu imefunguka, na wakashuhudia Malaika sabiini alfu ambao hawakuwahi kushuka ardhini kabla yake, hakika amezikwa na wakaondoka.”** [Hii imepokewa na Haakim na kusahihishwa na al-Dhahabi. Imam Ahmad ameitaja kuwa yenye isnad hasan.]

Hakika, hadhi hii imetayarishwa na Mwenyezi Mungu (swt) kwa yule aliyetoa Nusra kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), wakati alipoisimamisha Dola ya Kiislamu. Hadhi hii ni sawa na huenda, kwa uweza wa Mwenyezi Mungu, ikawa ni kubwa zaidi kwa wale wanaotoa Nusra kwa Waislamu katika zama hizi. Ni wakati ambapo Uislamu haupo katika maisha yao, na huku nguvu ya ukafiri na ukatili ikiwazonga, maadui wanajikusanya dhidi yao na mifumo yote na amri zinawagonga kwa kuwafikiana. Hivyo, yule aliyefuzu miongoni mwa Watu Wenye nguvu na Kinga ni yule aliyeitumia fursa hii, ambayo imejitokeza baada ya karne kumi na nne kwa mara ya pili. Mwenye kufuzu anahangaikia kuipata zawadi hii na hadhi ya yule aliyeipatiliza fursa kwa mara ya mwanzo, kiongozi wetu, Sa’ad bin Muadh (ra).

Ama kwa yule aliyenyimwa miongoni mwa Watu wenye Nguvu na Kinga, ni yule aliyeiuza Akhera yake kwa Dunia, au Akhera kwa Dunia ya mwengine. Huyu anahangaikia medali, vyeo na nafasi kubwa kubwa katika jeshi la Waislamu. Hawekezi haya katika kuunusuru Uislamu na Waislamu, na kusimamisha hukmu za Sharia za Mola wa walimwengu wote hapa duniani. Badala yake anayafanya haya ili kupata fungu kubwa zaidi la starehe za dunia, na majivuno ya muda mfupi. Anasahau kuwa medali na vyeo havitomkinga na ghadhabu za Mwenyezi Mungu (swt), wala kwa chochote chengine kutokana na moto wa Jahannam, kama atashindwa kutoa Nusra kwa Dini hii.

Afisa mwenye kumiliki nguvu na kinga lazima atambue kuwa Sa’ad bin Muadh (ra) alikuwa ni binadamu kama sisi. Alikuwa na ghariza za kibinadamu ambazo sisi pia tunazo. Alikuwa na misukumo ya ghariza ya kumiliki, ya kizazi na ya kuishi, ambazo dhihirisho lake ni mapenzi ya pesa, hadhi, watoto na wanawake… Hata hivyo, kwa sababu imani yake ilikuwa safi na ya wazi, alikuwa na hakika kuwa starehe za dunia hii ni starehe za kupita tu. Alikuwa na hakika kuwa starehe za Akhera ni za kudumu na hazikatiki, na hizo ndio starehe halisi. Wenye kumiliki Nguvu na Kinga hivi leo lazima watambue kuwa Swahaba Sa’ad (ra) sio katika wasiofanikiwa katika historia ambapo lazima isijirejee. Kama alivyokuwa Saad (ra), wao pia wanaweza kufanya matendo yake mazuri, kwa kuwa Nusra yao ni kama Nusra yake. Kutajwa kwao leo ni sawa na tamko la wahyi la jana, kwa Sa’ad (ra).

Kutoka kwa Asim bin Qatada, imepokewa kuwa, “Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alilala, na Malaika alimjia – au Jibril alisema – wakati alipoamka, na kusema, من رجل من أمتك مات الليلة، استبشر بموته أهل السماء “Ni mtu gani kutoka Ummah wako aliyefariki usiku huu, ambaye maisha ya baada ya kifo chake yanafurahiwa na walioko mbinguni? Alisema, **لا أَعْلَمُ إِلا أَنَّ سَعْداً أَمْسَى دَنِفاً (مريضاً). مَا فَعَلَ سَعْدٌ؟ “Sijui, isipokuwa ni kwamba Sa’ad alipatwa na maradhi, Sa’ad amefanya nini?”** Walisema, يا رسول الله، قد قبض، وجاءه قومه فاحتملوه إلى ديارهم “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), roho yake imeshachukuliwa. Watu wake wamekuja kumchukua na kwenda naye majumbani mwao.” Mtume (saw) aliswali swala ya asubuhi na kwenda pamoja na watu. Watu walitembea kwa haraka, hadi viatu vyao kuwavuka, na majoho yao kuwavuka. Mtu mmoja akasema, “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), watu wamechoka.” Mtume (saw) alisema,

**إِنِّي أَخْشَى أَنْ تَسْبِقَنَا إِلَيْهِ الْمَلَائِكَةُ كَمَا سَبَقَتْنَا إِلَى حَنْظَلَةَ “Ninahofia Malaika watatutangulia kama walivyotutangulia kwa Handhwalah (ra).”** Alikuwa akirejea, **هَنِيئاً لَك أَبَا عَمْرٍو! هَنِيئاً لَك أَبَا عَمْرٍو “Hongera ewe Abu Umar! Hongera ewe Abu Umar!”**

Enyi Mnaomiliki Nguvu na Kinga miongoni mwa Maafisa wa majeshi ya Kiislamu! Hiki ndicho kipindi ambapo azma imetambulika, na matukufu yamenakiliwa. Hiki ndicho kipindi ambapo hamtapoteza kitu katika kutoa Nusra kwa Dini hii. Hivyo msipoteze fursa hii. Tekelezeni maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt) kwa tamko thabit, “Tupo kwa ajili yako, Ewe Mwenyezi Mungu, tupo kwa ajili yako”. Hivi leo, Ummah wa Kiislamu unakulilieni, basi itikieni kwa kusema, “Sisi ndio faraja yenu, enyi Ummah wetu, sisi ndio tulizo lenu.” Leo, Hizb ut Tahrir imenyosha mikono yake kwenu ili mlimalize jukumu lenu pamoja nayo, basi itikieni kwa kauli, “Sisi ndio Sa’ad wenu, Hizb ut Tahrir, sisi ndio Sa’ad.” Muitikieni yule anayekuitieni kwenye maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt)… Hamtaki kuwa katika njia ya Sa’ad wawili, Sa’ad bin Muadh na Sa’ad bin Ubadah, As’ad na Usayd?! Hamtaki kituo chenu kuwa kama kituo chao, na kupanda kufikia kituo chao, kupata starehe za kudumu kama zao?!

Enyi Mnaomiliki Nguvu na Kinga miongoni mwa Maafisa wa majeshi ya Waislamu! Msimamo wa kiongozi wa Ansar, Sa’ad bin Muadh (ra), ulijaza furaha nyoyoni mwa Waislamu. Jina lake halitajwi, isipokuwa ndimi zinakuwa na furaha kwa kumuombea Dua. Haijasikika Arshi ya

***Endelea... UK 4***

Aliyetukuka ikitingishika kwa kifo chake, isipokuwa macho yakibubujikwa na machozi ya furaha kwa ajili yake, kukiwa na shauku kubwa ya kuyapata mfano wa hayo. Je kuna njia nyengine ya kurejea kwa Mola wetu (swt)?! Utukufu wa watu upo kwenye misimamo yao, kwa hali yoyote iwayo, kukiwa na msisitizo wa kuyafikia, licha ya kila aina ya changamoto iliyopo… Mnaishi katika wakati ambao, wito sawa na ule wa Muhajirun kwa Ansar unatolewa kwa mara nyengine. Kwa hiyo, kuweni Ansar wetu hivi leo. Nyanyueni utukufu wa Dini yetu. Nyanyueni utukufu wa Ummah wetu.

Tunajua kwa yote haya, kama mjuavyo. Mahala penu stahiki ni juu ya viwanja vya mapambano. Basi viko wapi viwanja vya mapambano ya utukufu ambavyo watawala hawa wamefungua kwa ajili yenu?! Viko wapi vita vya heshima ambavyo wamepigana pamoja nanyi?! Viko wapi vita vya kishujaa, ambavyo majina yenu na matendo mazuri yamehifadhiwa?! Viko wapi vita ambavyo nyinyi mnatambulika navyo, na kutambulika nanyi? Tunajua, kama mjuavyo, kuwa nyinyi si tu waajiriwa. Jukumu lenu sio tu utulivu na kuhifadhi maisha. Nyinyi ni ufunguo wa milango ya muendelezo katika utawala na uwezeshaji katika mamlaka. Nyinyi ni jukwaa la Umma kwa ajili ya Jihad dhidi ya maadui wa Dini. Ummah unahitaji kukuoneni mkiwa kama Musa bin Nasir, Uqba bin Nafi’, Muhammad bin Qasim na Tariq bin Ziyad.

Mnafahamu, Enyi Watu wa Nusra Yetu, kuwa watawala hawa wanataka kushinda kwa ushawishi wao, na kubakia katika udhalimu wao. Wanakutakeni kusimama pamoja nao na kulinda uongo wao. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu (swt) anakutakeni kuchukua mamlaka kutoka kwa watu hawa. Mwenyezi Mungu (swt) anakutakeni kuwapatia mamlaka ya utawala watu wa Da’wah, kusimamisha Khilafah Rashida ya Pili kwa njia ya Utume, ili watawale kwa yale yote ambayo Mwenyezi Mungu (swt) ametushushia. Watawala hawa wanajuwa kuwa miongoni mwenu kuna wanyenyekevu wanaoheshimu Dini yao. Wanajua kuwa miongoni mwenu kuna wenye hasira nao, kwa sababu ya miamala yao ya aibu na maafikiano. Wanajua kuwa miongoni mwenu kuna ambao hisia zao zinatingishika kwa kile ambacho Ummah unakabiliana nacho chini ya mikono ya maadui zao, pamoja na wale wanaopatwa na maumivu wanayoyahisi Waislamu…

Kwa hiyo, wanakutisheni, wanakutengeni, wanakuchunguzeni, wanakubaneni, wanakubadilisheni vyeo vyenu na kukuhojini. Wanampandisha cheo afisa mwenye fikra ya uovu, huku wakikataa kumpandisha cheo afisa mwenye kuheshimika, aliyetengenea. Wanafanya hayo kufadhaisha uwezo wenu katika kuleta mabadiliko, wakati Mwenyezi Mungu (swt) anakutakeni kuwatwaa watawala, kuwachapa migongo yao, kuwang’oa, na kuuepusha Ummah kutokana na uovu wao. Mwenyezi Mungu (swt) anakutakeni kuwa wenye nguvu dhidi ya watawala waovu, wenye huruma kwa Waislamu, na walinzi wa Dini hii. Huu sio muda wa kusitasita, wala sio muda wa kuchelewa chelewa. Huu ni muda wa haki kwa Ummah na Nusrah kwa Dini hii. Kama hamtotoa kipaumbele kwa maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume Wake (saw) juu ya masuala ya uovu, hali ngumu itabakia kwa Dini yenu na Ummah wenu. Na mambo yatageuka dhidi yenu Akhera, kwa kupuuza kwenu.

Hivyo je Sa’ad (ra) angeweza kukubali kile ambacho Mayahudi wanafanya kwa Waislamu Palestina? Au Marekani ilivyofanya Iraq na Afghanistan, pamoja na uadui wake wa uvamizi dhidi ya Waislamu kila mahali? Au kile Urusi ilichofanya Chechnya na Syria, India katika Kashmir, na China katika Turkestan Mashariki?! Basi kwa vipi, vizazi vya Sa’ad vinayakubali haya yote? Hatuwageukii waovu miongoni mwa wanaomiliki nguvu miongoni mwenu, ambao ni sawa na watawala. Tunawageukia walio wakweli miongoni mwenu. Hatutaki Nusrah isipokuwa kutoka kwa walio na mfano wenu. Kwa hiyo, hamna sababu ya kukataa. Hamna sababu ya kubakia kimya na kutulia tu. Kama hamtochukua hatua ya kutoa Nusrah kwa Dini yetu, basi nani atachukua hatua hiyo?

Kubadilisha watawala wa leo, ili kusimamisha hukmu kwa yote yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu (swt), ni suala muhimu zaidi ya maagizo yote katika Dini. Mabadiliko haya ya kivitendo yapo chini ya mabega ya wenye kumiliki nguvu, kabla ya wengine wote. Njia zimeandaliwa kwa ajili yenu, ili mahitaji ya Ummah yawe ni kubadilisha watawala. Njia zimeandaliwa kwa ajili yenu, kiasi kwamba watawala wanahofia kisasi cha wananchi juu yao. Njia zimeandaliwa, kiasi kwamba upanga wa wavamizi wa Marekani na Ulaya umevunjika chini ya fuawe ya mujahidina, huku makamanda wa Kiyahudi wameanza kugundua hofu yao ya kuibuka kwa Salahuddin hivi sasa.

Njia zimefunguliwa na zinawasubiri wale watakaopita kuelekea kwenye Haki. Toeni Nusra yenu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (swt). Bishara njema ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ya Khilafah ya pili kwa njia ya Utume inakusubirini. Kuweni Ansar wa leo mtakaotoa Nusra ya kurejea kwake. Kuweni akina Sa’ad wa Ummah huu hivi leo. Sa’ad yupo miongoni mwenu, basi na ajitokeze. Ummah una hamu ya kumuona miongoni mwenu. Unamsubiri Sa’ad kuchukua mamlaka, juu ya Haki, kuiweka ikiwa ni amana kwa watu wanyenyekevu wa Da’wah, ili wasimamishe Khilafah Rashida ya Pili kwa Njia ya Utume, kuhukumu kwa Haki. Mwenyezi Mungu (swt) anasema,

مَنْ كَانَ يَظُنُّ أَنْ لَنْ يَنْصُرَهُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ فَلْيَمْدُدْ بِسَبَبٍ إِلَى السَّمَاءِ ثُمَّ لِيَقْطَعْ فَلْيَنْظُرْ هَلْ يُذْهِبَنَّ كَيْدُهُ مَا يَغِيظُ

**“Anayedhani kwamba Mwenyezi Mungu hatamnusuru (Mtume) katika dunia na Akhera na afunge kamba kwenye dari kisha aikate. Atazame je hila yake itaondoa hayo yaliyo mkasirisha?.”**
[Surah Al-Hajj 22:15]

## HABARI NA MAONI

# Ni Uislamu Tu Ndio Wenye Suluhisho la Kweli kwa Usalama wa Chakula kwa Afrika




**Habari:**

Kuanzia Septemba 5 hadi 8, 2023 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa 13 wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika. Mkutano huo ulioendeshwa ana kwa ana, na mtandaoni ulikuwa na wazungumzaji zaidi ya 350, zaidi ya wahudhuriaji 3,000 kutoka zaidi ya nchi zaidi 70. Mkutano huo ulibeba kauli mbiu: "Huisha, Tengeneza, Chukua hatua kwa Suluhisho la Afrika kwa Mabadiliko ya Mifumo ya Chakula". Mkutano huo ulilenga kurudisha mifumo bora ya chakula na kujitosheleza ukiwalenga vijana na wanawake kama sehemu muhimu.

**Maoni:**

Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika – AGRF ni jukwaa kuu la Kiafrika la mifumo ya kilimo na chakula, linaloleta pamoja wadau kuchukua hatua za kivitendo na kujifunza kwa pamoja jinsi ya kuimarisha na kupeleka mbele mifumo ya chakula ya Afrika.

Kwa mujibu wa kaulimbiu ya jukwaa hilo la AGRF, tamko 'Kuhuisha', linamaanisha kutandika mikakati thabiti na hatua za kivitendo za kujenga upya mifumo ya chakula, 'Kutengeneza' kunakusudiwa uwepo wa haja ya kuzalisha upya rasilimali asilia kivitendo, uvumbuzi, na teknolojia kwa ajili ya uzalishaji endelevu wa chakula katika mazingira ya mabadiliko ya hali ya hewa. Amma tamko 'Kuchukua hatua' kunalenga kujifunga na hatua za haraka kuharakisha gurudumu la mabadiliko ya mifumo ya chakula kupitia sera bora, kwa matendo na uwekezaji.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Afrika, Afrika ina takriban hekta milioni 874 za ardhi ambayo inafaa kwa kilimo, 83% ina udongo wenye rutuba ya kutosha na wenye uwezo wa kufikia uzalishaji wa hali ya juu na endelevu. Pia, (Afrika) ina zaidi ya mito 67 mikubwa na mabonde 63 ya mito inayovuka mipaka. Kwa ufupi, 65% ya ardhi inayolimwa duniani na 19% ya maji safi yanayoweza kuregeshwa duniani yanapatikana barani Afrika.

Kuhusiana na vyakula vya baharini, nchi 27 za Afrika zinapakana na Bahari ya Atlantiki, 13 zinapakana na Bahari Hindi, 5 zinapakana na Bahari ya Mediterania na 4 zinapakana na Bahari Nyekundu.

Kwa upande wa rasilimali watu, Afrika ni makaazi ya watu bilioni 1.3 miongoni mwao karibu 70% ni vijana chini ya miaka 30. Zaidi ya hayo Afrika ina 40% ya dhahabu duniani, 90% ya madini ya kromiamu na platinamu na mrundikano mkubwa wa akiba kubwa ya kolbati na urani inapatikana katika Afrika.

Licha ya rasilimali zote hizo, Afrika bado inakabiliwa na uhaba wa chakula, njaa na ukame. Zaidi ya watu milioni 140 barani Afrika wana njaa, Somalia hivi karibuni imefikia kiwango cha kutisha ikikadiriwa kuwa na watu milioni 6.5 wanaokabiliwa na shida ya chakula, watu milioni 17.5 hawana chakula cha kutosha nchini Nigeria, nchini Madagascar watu milioni 7.8 wanakabiliwa na uhaba wa chakula, na watu milioni 22.7 nchini Ethiopia hawana uhakika wa chakula. Ukanda wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni mojawapo ya sehemu

***Endelea... UK 6***

hatarishi katika majanga ya chakula yanayotisha zaidi katika miongo kadhaa ambapo takriban watu milioni 146 wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula. Katika bara la Afrika, njaa inachangia hadi 45% ya vifo vya watoto.

Mkutano wa Jukwaa la Mfumo wa Chakula Afrika, kama yalivyo majukwaa mengine halitofanikiwa kulinda Afrika na dunia kutokana na njaa na uhaba wa chakula, kwa sababu mipango yote haijafikia chanzo halisi cha mgogoro wa chakula barani Afrika. Na lau mipango hiyo ingefikia chanzo (cha tatizo) basi wangeweza kuja na suluhisho muwafaka. Badala yake wanapendekeza masuluhisho ya kibepari na kufikiria ndani ya mipaka ya ubepari, kutegemea masuluhisho ya kikoloni ya Wamagharibi kutatua matatizo yaliyoletwa na hao (Wamagharibi).

Mabadiliko ya hali ya hewa barani Afrika yanachangiwa sana na viwanda vya kibepari vya wakoloni wa Magharibi vinavyosababisha hali mbaya ya hewa na kusababisha majanga yanayoathiri mfumo wa chakula ambayo kwa sasa yanatokea kila baada ya miaka 2.5, hali hii ni mara nyingi zaidi kuliko hapo awali.

Afrika inakabiliwa na ongezeko la bei ya chakula, na bei ya chini na duni kwa bidhaa zao za kilimo katika soko la dunia kutokana na mfumo wa kiuchumi wa kikoloni ambao Afrika imefanywa kuwa shamba la Wamagharibi ambapo wakoloni huja na kunyonya rasilimali na kuendelea kuifanya Afrika kuwa maskini zaidi duniani.

Iwapo Afrika itasimamiwa vyema, sekta yake ya kilimo inaweza kutatua sio tu mgogoro wa chakula ndani ya Afrika, bali ulimwengu kwa jumla, na hilo linawezekana tu kupitia Uislamu pekee.

Chini ya dola ya Kiislamu (Khilafah), mataifa ya kikoloni ya Magharibi hayatokuwa na fursa yoyote ya kudhibiti sera, mipango na programu zetu za kilimo. Sera za Kiislamu za kilimo kama vile kuzingatia kulisha wahitaji kuwa jambo la lazima (faradhi), kufufua ardhi zilizokufa, usambazaji thabiti wa chakula, kufadhili miradi midogo na mikubwa ya kilimo nk. Sera hizo za kujitegemea, zisizotegemea nchi za Magharibi zitahakikisha uzalishaji wa chakula kwa wingi, kuongeza uwezo wa kilimo wa Ummah kama vile viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na kilimo, kwa ajili ya kulisha wenye njaa na kutengeneza ajira.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**
**Mjumbe wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

Afisi ya Habari
Wilayah Syria

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 02/1445 | Jumapili, 25 Safar 1445 H | 10/09/2023 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Ushawishi wenye Sumu wa Marekani na Athari Zake Mbaya

Mnamo Agosti 27, 2023, uongozi wa yale yanayojulikana kama SDF (Majeshi ya Kidemokrasia ya Syria), pia yanayojulikana kama QSD, yalimkamata kiongozi wa baraza la jeshi la Deir Ez-Zor baada ya kumvutia, pamoja na baadhi ya makamanda wake, kwenye mkutano mmoja katika kambi ya Waziri huko Al-Hasakah. Kitendo hiki cha udanganyifu kilifanywa na Mazloum Abdi, na baraza la jeshi la Deir Ez-Zor lilikuwa moja ya vitengo vya Kiarabu ambavyo vilikuwa sehemu ya SDF.

Kabla ya tukio hili, kutokubaliana kulitokea kati ya makundi mawili, ambako kulitatuliwa kupitia upatanishi wa majeshi ya Marekani.

Kufuatia kukamatwa kwa Ahmed al-Khubayl, anayejulikana pia kama Abu Khawla, kiongozi wa baraza la jeshi la Deir Ez-Zor, kabila lake lilihamasishwa kudai kuachiliwa kwake. Wito wa kutaka hatua za kijeshi kuchukuliwa dhidi ya Wakurdi walio ndani ya safu za SDF ulipaza sauti zaidi, na maombi yalifanywa kwa Waarabu walio ndani ya SDF kujiuzulu. Hata hivyo, miito hii ilipokea machache.

Ni dhahiri kwamba mkorogo wa Marekani na uingiliaji kati wake wenye sumu ndio sababu ya shida hizi zote. Matokeo ya vitendo hivi ni hatari sio tu kwa umoja wa watu lakini pia kwa utulivu wa eneo. Eneo hili linatamani amani na umoja, likiwa huru kutokana na uingiliaji kati na ajenda za kigeni.

Watoto wa maeneo yaliyokombolewa kaskazini na kaskazini magharibi, wanaosimamiwa na Uturuki, wamejibu kile kinachotokea katika maeneo yanayodhibitiwa na SDF (Majeshi ya Kidemokrasia ya Syria), ambayo yanasimamiwa moja kwa moja na Marekani.

Katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia mwisho wa matukio haya na kurudi kwa vikosi vya SDF kwenda maeneo ya mashariki mwa Mto Furat. Lakini, kile kilichotokea ni hatua ya kwanza katika mpango wa Marekani wa kukuza mgawanyiko kati ya Waarabu na Wakurdi na kuwaangazia viongozi wa Kiarabu wanaohusiana nao, wenye uwezo wa kutekeleza njama zao za kisiasa.

Kama ndugu zenu katika Hizb ut Tahrir ambayo inabaki kuwa chama kinachoongoza ambacho hakiwadanganyi watu wake, na imekuwa na uzoefu na kujulikana na nyinyi katika miaka yote ya Mapinduzi, hatujasaza juhudi yoyote katika kutoa ushauri na kufichua hatari na njama dhidi ya mapinduzi ya Ash-Sham. Hivyo basi, ni wajibu kwetu kuwashauri watu wetu na kutoa mwanga juu ya ukweli fulani, tukitumaini kuwa utatumika kama funzo kwa siku zijazo, inshallah.

1- Ni nipi kilichotokea katika majimbo ya Furat Mashariki chini ya macho na masikio ya vikosi vya Marekani?
Wao ndio waliowapa nguvu viongozi na watu wa vyama vya kujitenga vya Kikurdi, pamoja na PKK, na wengine katika jimbo hilo lenye idadi ya Waarabu, kuwafanya washirika katika vita vyao dhidi ya 'ugaidi' na kuwawezesha kudhulumu na kukandamiza watu.

Lau ingetaka kukomesha utawala na ukandamizaji wao, ingeweza kufanya hivyo. Lakini, ni Marekani yenyewe ndiyo iliyoruhusu hili kutokea, ikiruhusu mapigano ya hivi karibuni kufanywa ndani ya masikio na macho yake. Hili limeongeza uhasama na chuki kati ya Waarabu na Wakurdi, kwani linaanza kuchora mipaka ya umwagaji damu, likitaka kutenganisha watoto wa taifa moja.

2- Vyama vya Kikurdi vya kujitenga vilivyo madarakani haviwakilishi ndugu zetu wa Kikurdi. Vyama hivi vimejiweka katika huduma ya Marekani na mataifa mengine ya ulaji njama dhidi ya Ummah. Ni ala duni mikononi mwa nchi hizi, zilizodanganywa kwa miaka mingi na bado zinatumika kama silaha hatari dhidi ya vipote vya Wakurdi na Waarabu.

*Endelea... UK 8*

Suala sio, kama ambavyo Marekani ingependa iwe, mapigano kati ya Wakurdi na Waarabu; Badala yake, ni mapambano kati ya waliokandamizwa na wenye kukandamiza, kwa msaada wa Marekani kwa malengo maovu.

3- Imedhihirika wazi kwamba uongozi wa Baraza la Kijeshi la Deir ez-Zor umejitenga na uungwaji mkono wa wananchi, sawa na viongozi wengine ndani ya mfumo wa makundi. Wametumia nyadhifa zao, ambazo zilijengwa juu ya damu ya mashahidi na mihanga ya wanamapinduzi, kwa ukandamizaji, utawala, na uvamizi dhidi ya watu wa mapinduzi. Viongozi hawa walipewa dhamana ya kubeba mwenge wa mapinduzi, kuindoa dhulma kutoka kwa watu wao, na kufikia malengo ya uasi wao. Lakini, badala yake, wamekuwa ni ala duni mikononi mwa mataifa yanayo kula njama dhidi ya watu wao wenyewe. Wametoa kwa hamu utiifu kamili kwa mabwana zao, na hivyo kupoteza huruma, uungwaji mkono, na umoja wa watu katika nyakati magumu.

4- Baadhi ya viongozi wa kikabila ambao wamechukua hatua dhidi ya vikosi vya SDF wameanza kutafuta suluhu kutoka kwa Marekani na vikosi vya muungano, na kusahau kwamba Marekani ni mfadhili wa utawala wa uhalifu na muungaji mkono wa mashirika ya Kikurdi yaliyojitenga. Ni nyuma ya njama zote zilizopangwa dhidi ya Mapinduzi ya Ash-Sham, ikiwa ni pamoja na suluhisho lake la kisiasa lenye sumu na azimio hatari la kimataifa nambari 2254, ambalo linalenga kukandamiza mapinduzi ya Syria na watoto wake wanyoofu. Je, mapinduzi yatashinda vipi wakati yanatafuta suluhu na uungwaji mkono na wale wanaokula njama dhidi yake mchana na usiku?

5- Harakati za kweli za watu na wito wa dhati wa kuomba msaada ambao umeenea katika maeneo yote yaliyokombolewa ni matendo yenye baraka, yanayoonyesha asili ya kina ya mapinduzi ndani ya nyoyo za watoto wake. Inaonyesha kuwa mapinduzi bado yanawaka ndani yao, licha ya njama za kishetani na njama kubwa zinazofanywa na mataifa yenye uadui na ala zao duni dhidi ya Mapinduzi ya Ash-Sham na watu wake waaminifu.

Hata hivyo, miito hii ya wananchi isiyo na mpangilio imethibitisha hitaji la dharura la kuwepo kwa uongozi wa kisiasa wa dhati na makini unaoweza kuzuia juhudi hizi kutoka katika malengo yao na kukwamisha mipango ya wale wanaotaka kunyonya mienendo ya wananchi kwa mipango ya njama zao. Ni muhimu kuziimarisha harakati hizi za dhati kwa mwamko wa kisiasa, kuzifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pekee na kuinusuru Dini Yake na wanaodhulumiwa miongoni mwa waja Wake.

Zaidi ya hayo, mujahidina lazima waasisi uongozi wa kijeshi wa dhati na wenye uzoefu, wenye jukumu la kupanga juhudi zao na kupanga mipango ifaayo kwa ajili ya vita vya maamuzi na vyenye athari. Hii inahakikisha kwamba hakuna mtu anayewaongoza watu katika vita vya pembeni ambavyo vinamaliza juhudi za wanyoofu na kupanda ukataji tamaa katika nyoyo zao, na kuwapelekea kukubali suluhisho lolote la njama lililowekwa juu ya Mapinduzi ya Ash-Sham. Hili ni sawa na vile watawala wasaliti walikuwa wakifanya kwa kuonyesha kutokuwa na uwezo wa majeshi yao kukabiliana na umbile nyakuzi la Kiyahudi.

Amali za kijeshi zinahitaji mipango na mpangilio sahihi, na lazima ziimarishwe na ufahamu wa uongozi wa kisiasa. Yote haya ni muhimu ili kufikia misingi thabiti ya mapinduzi ya Ash-Sham, ya kwanza kabisa miongoni mwao ikiwa ni kupinduliwa kwa utawala wa kihalifu, katiba yake, nguzo zake zote, nembo zake, na kusimamisha utawala wa Kiislamu juu ya magofu yake.

6- Imethibitika pasi na shaka, kwamba sababu ya kurudi nyuma na kukata tamaa kulikoyapata Mapinduzi ya Ash-Sham baada ya kuanzishwa kwake kwa baraka na udhibiti wake juu ya zaidi ya 80% ya ardhi ya Syria ni kwamba yalikubali msaada na pesa chafu za kisiasa kutoka nje. Hili liliufunga uongozi kwa wafuasi, ambao ulitupora uamuzi wa mapinduzi, ukageuza mkondo wake, na kuyaweka kwenye hila za maadui zetu.

Hakuna wokovu kwetu kutokana na hali yetu ya sasa isipokuwa kwa kukata mikono ya wafuasi, kukataa masuluhisho ya wenye chuki, na kushikamana na kamba yenye nguvu ya Mwenyezi Mungu peke yake. Tunapaswa kuweka tumaini letu Kwake kuinusuru Dini Yake na kuliheshimu Neno Lake kupitia kutabanni mradi mtukufu wa Kiislamu wa kutabikisha mfumo na sheria Zake chini ya kivuli cha Khilafah Rashida kwa njia ya Utume. Hebu natumwamini Mwenyezi Mungu ili atujaalie kufaulu, hebu na tumnusuru Mwenyezi Mungu ambaye mikononi mwake Peke Yake umo ushindi, ili Mwenyezi Mungu atujaalie ushindi na atutimizie ahadi yake kama alivyosema Yeye, Mtukufu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ

**“Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu.”** [Surat Muhammad:7]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Syria**

# HABARI NA MAONI
# Vladimir Putin Amechukua Mahali pa Karimov



**Habari:**

**Mnamo tarehe 11 Agosti, shirika la habari la RIA Novosti liliripoti:** *"Muungano wa gesi tatu wa Urusi, Uzbekistan na Kazakhstan huenda ukapanuliwa ili kujumuisha nchi zengine, Dmitry Birichevsky, mkurugenzi wa Idara ya Ushirikiano wa Kiuchumi ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Urusi, aliiambia RIA Novosti.*

*Hatuondoi uwezekano wa kupanua ushirikiano wa pande tatu katika sekta ya gesi. Tunajua kuwa dola zengine pia zinavutiwa nao. Tuko wazi kwa ushirikiano kama huo kwa kuelewa kwamba unapaswa kuwa na manufaa na kujenga, kwa kuzingatia nafasi za washiriki wote,"* alisema.

**Maoni:**

Kulingana na data ya OPEC ya 2021, Uzbekistan ilishika nafasi ya 17 kwenye orodha ya nchi kwa suala la uzalishaji wa gesi kwa mwaka, huku Urusi ikishika nafasi ya 2. Pamoja na hayo, Urusi, baada ya uvamizi wa kijeshi dhidi ya Ukraine, imekuwa chini ya vikwazo, ambayo imepunguza kwa kiasi kikubwa usambazaji wa gesi kwa Ulaya na nchi nyingine. Na nchi za Ulaya zenyewe, licha ya haja ya gesi, zinaanza kukataa kununua gesi ya Urusi.

Mamlaka ya Kremlin katika medani ya kimataifa imeshuka hadi kufikia kiwango cha madikteta wa Asia ya Kati. Ziara ya mwisho ya Putin barani Ulaya ilikuwa Uswizi mnamo 2021. Leo Putin anacheza kwenye mazingira yasiyo na tija pamoja na wasaidizi wake, marais madikteta wa Uzbekistan, Kazakhstan na Tajikistan. Katika kipindi cha mwaka mmoja hivi uliopita kumekuwa hakuna habari kuhusu ziara ya Putin barani Ulaya au ziara ya viongozi wa Ulaya nchini Urusi. Putin alifukuzwa kutoka G8 na hakubaliwi tena barani Ulaya.

Sasa Kremlin inapaswa kuuza gesi yake ili kukwepa vikwazo kupitia Uzbekistan au Kazakhstan. Dhalimu Karimov, rais wa kwanza wa Uzbekistan, alikuwa akiuza gesi kwa njia hii. Wakati huo, Uzbekistan ilikuwa chini ya vikwazo, na Karimov alikuwa na hasira na ugomvi kila wakati na Kremlin kwa sababu Putin alikuwa akinunua gesi kwa bei ya chini na kisha kuiuza tena kwa Ulaya kwa bei ya juu zaidi. Sasa, Putin yumo ndani ya viatu vya Karimov na hawezi kuuza gesi Ulaya au nchi nyingine kwa sababu ya vikwazo.

Uzbekistan nayo inajihalalisha kwa jumuiya ya kimataifa kufanya biashara na Urusi kwa ukosefu wa gesi nchini humo, ingawa iko katika viongozi 20 wa juu katika uzalishaji wa gesi duniani. Haishangazi kwamba uwongo mbaya kama huo unawafaa viongozi wa serikali kuu za ulimwengu. Kwa sababu leo sera nzima ya jumuiya ya ulimwengu imejengwa juu ya udanganyifu na unafiki.

Katika Uislamu, gesi kama maliasili ni mali ya umma. Serikali au mtu binafsi hawezi kutumia maliasili hii na kuitumia kwa khiyari yake pekee. Imepokewa na Abu Dawud kutoka kwa Ibn Abbas kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

الْمُسْلِمُونَ شُرَكَاءُ فِي ثَلاَثٍ فِي الْمَاءِ وَالْكَلإِ وَالنَّارِ وَثَمَنُهُ حَرَامٌ

**"Waislamu ni washirika katika vitu vitatu: maji, malisho na moto".** Hadith hii hii imepokewa na Anas kwa ziada ya "...na mauzo yake ni haramu". Imepokewa na Ibn Majah kutoka kwa Abu Hurairah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema: ثَلاَثٌ لاَ يُمْنَعْنَ الْمَاءُ وَالْكَلأُ وَالنَّارُ **"Vitu vitatu havinyimwi watu: maji, malisho na moto."** Hii yaashiria kwamba watu ni washirika katika maji, malisho na moto na ni haramu kwa mtu binafsi kuchukua umiliki wa vitu hivi.

Ni Dola ya Khilafah Rashida ya Pili pekee inayoongozwa na mtawala mwadilifu ndiyo inayoweza kusitisha uuzaji wa gesi na kukomesha jinai za watawala wetu madhalimu na mabwana zao wakoloni. Tuna imani kuwa ahadi hii itakuwa kweli hivi karibuni, kwani Mwenyezi Mungu hutumiza ahadi zake. Na sisi tunamtegemea Mwenyezi Mungu!


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Eldar Khamzin**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Marekani iko katika “Mzunguko wa Kifo wa Kweli. Muda Unayoyoma!”



**Habari:**

Maoni yaliyochapishwa katika Wakfu wa Urithi wa kihafidhina mnamo tarehe 11 Agosti yenye kichwa "Kushindwa kulipa kwa Jina Jengine: Kwa Nini Deni la Marekani Linafaa Kupunguzwa."

**Maoni:**

Inafuatia kushushwa daraja kwa hivi majuzi kwa kiwango cha mikopo ya serikali ya Marekani kutoka AAA hadi AA+ na shirika la Fitch. Mwandishi wake anasema kwamba hakuna hatari inayowezekana ya kushindwa kulipa, "lakini haipaswi kupuuzwa." Deni la Marekani limevuka dolari trilioni 32, na linakua kwa kasi inayoongezeka. Lazima kuwe na kikomo kwa kiasi gani deni hilo linaweza kukua kabla ya kutoweza kuepukika. Maoni hayo yalibainisha kuwa “malipo ya riba pekee kwa deni hilo kubwa hutugharimu takriban $1 trilioni - zaidi ya bajeti yote ya Ulinzi - na matumizi yanaendelea kukua. Hicho ni kichocheo cha kufilisika na hatimaye kushindwa kulipa.”

Kushindwa kudhibiti deni kutairegesha Marekani "moja kwa moja hadi kwenye kasi ya mfumko wa bei na kushindwa kulipa kulikojificha kwenye deni la Marekani." Matokeo yatakuwa “mavuno mengi zaidi, ambayo husababisha malipo ya juu zaidi ya riba, ambayo yanamaanisha hata deni linalokua kwa kasi zaidi, na kadhalika—mzunguko wa kifo cha kweli. Muda unayoyoma kabla tufikie hatua ya kutorudi tena.”

Neno ‘kushindwa kulipa kulikojificha’ kunakusudia ukweli kwamba ingawa watu binafsi au makampuni hushindwa kulipa madeni yao waziwazi, serikali zinaweza “kuongeza deni lao kwa kupunguza thamani ya sarafu zao.” Maoni ya Heritage yanaonya kuwa Biden anafanya hivyo hasa huku dolari ikiwa imepunguzwa thamani kwa 16% kuanzia uraisi wake hadi sasa.

Hifadhi ya Shirikisho imekuwa ikijaribu kudhibiti mfumko wa bei tangu mwisho wa 2021, lakini mfumko wa bei bado ni wa juu zaidi kuliko 2% iliyolengwa. Wakati huo huo Marekani inaendelea kutumia kile isichokuwa nacho na hatimaye mtu atalazimika kulipia gharama ya hilo.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Dkt. Abdullah Robin**




**Swali:**

Assalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakatuhu Sheikh wetu mpendwa

Namuomba Mwenyezi Mungu akupe nguvu, akupe afya na umri mrefu na akujaalie kushuhudia kurudi kwa Khilafah na utuongoze, Amin.

Nina swali kuhusiana na rasimu ya katiba ya Hizb. Katika ibara ya 7 kifungu cha F inasema: "Dola itatabikisha hukmu zote za Sharia na mambo yote ya Shari'ah ya Kiislamu, kama vile miamala, kanuni za adhabu, ushahidi, mifumo ya utawala na uchumi miongoni mwa mengine kwa usawa juu ya Waislamu na Wasiokuwa Waislamu, Dola pia itatabikisha hayo hayo juu ya wale walio na mkataba, wanaomba hifadhi na wale wote walio chini ya mamlaka ya Uislamu kwa njia hiyo hiyo. Inatabikisha kwa wanajamii wote isipokuwa kwa mabalozi, wajumbe na mithili yao kwa kuwa wana kinga ya kidiplomasia."

Swali langu ni kuhusu hoja kuhusu Mabalozi. Uhalisia ni kwamba wakati mwingine kuna mabalozi wa muda ambao hukaa kwa muda tu kisha kurudi kwenye nchi zao na mabalozi wa kudumu ambao hukaa ndani ya Khilafah kwa kudumu. Je, kifungu hiki kinahusu aina zote mbili za mabalozi?

Pia, endapo mmoja wa balozi atafanya uhalifu au kufanya shughuli isiyo halali nje ya mipaka yao kama mabalozi, je, wote wawili watahukumiwa na kuadhibiwa ipasavyo na Khilafah? Au mabalozi wa muda na wa kudumu wanachukuliwa tofauti katika jambo hili.

Jazakumullahu Khairan.

Kutoka kwa: Saifudeen Abdullah

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Baraka za Mwenyezi Mungu ziwe nawe kwa dua yako nzuri kwangu, pia namuomba Mwenyezi Mungu akupe kheri.

1- Kuhusiana na swali lako kuhusu mabalozi wa kudumu na wa muda. Hakuna tofauti baina yao katika mtazamo wa Shariah, maadamu maana ya neno (mjumbe) inatumika kwa mtu huyo, anakuwa na kinga ya kidiplomasia wakati wa kukaa kwake ndani ya dola ya Khilafah, bila ya tofauti yoyote... Hapo awali, katika zama za Mtume (saw), Maswahaba na zama zilizofuata, hapakuwa na mabalozi wa kudumu na wakaazi. Badala yake, wajumbe walitumwa kufikisha ujumbe na kisha kurudi katika nchi yao, yaani, walikuwa, kulingana na usemi wako (mabalozi wa muda / wajumbe wa muda) ... Kisha mabalozi na afisi za mabalozi za kudumu duniani zikaanzishwa kutokana na uzito wa mahusiano na haja ya mawasiliano ya kudumu kati ya nchi na uwepo wa raia wa ubalozi wa nchi hizo ndani ya nchi husika. Kwa hiyo, dola zilianza kukubali kufunguliwa kwa afisi za ubalozi za kudumu za nchi nyingine katika ardhi zao na kukubali kibali cha mabalozi wa nchi hizo wanaoishi ndani yake... Zamani balozi au mjumbe alikuwa akienda mara moja tu kupeleka ujumbe mahususi... Hili ndilo linalofahamika kutoka kwa Hadith tukufu kuhusiana na wajumbe, kama alivyosimulia Ahmad kutoka kwa Ibn Masoud ambaye amesema:

**جَاءَ ابْنُ النَّوَّاحَةِ وَابْنُ أُثَالٍ، رَسُولاَ مُسَيْلِمَةَ إِلَى النَّبِيِّ ﷺ، فَقَالَ لَهُمَا: أَتَشْهَدَانِ أَنِّي رَسُولُ اللَّهِ؟ قَالاَ: نَشْهَدُ أَنَّ مُسَيْلِمَةَ رَسُولُ اللَّهِ، فَقَالَ النَّبِيُّ ﷺ: آمَنْتُ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ، لَوْ كُنْتُ قَاتِلاً رَسُولاً لَقَتَلْتُكُمَا، قَالَ عَبْدُ اللَّهِ: قَالَ: فَمَضَتِ السُّنَّةُ أَنَّ الرُّسُلَ لاَ تُقْتَلُ**

***Endelea... UK 12***

Ibn Nawwaha na Ibn Uthal walikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kama wajumbe Musaylama - mrongo - na Mtume wa Mwenyezi Mungu akawaambia: **“Je, mnashuhudia kwamba mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu?”** Wakasema: “Tunashuhudia kwamba Musaylama ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.” Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: Mimi ninamuamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake. “Mimi nakupeni usalama kupitia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kama ingekuwa mimi ni mwenye kumuua mjumbe ningekuuweni nyinyi wawili.” Abdullah amesema: dhihirisho la sunna hii ni kwamba wajumbe hawauwawi.” (Imepokewa na Ahmad na kutangazwa kuwa ni Hasan na Al-Haythami).

Ni wazi kutokana na Hadith hii kwamba hotuba hiyo inahusu wajumbe wawili waliotumwa kutoka kwa Musaylamah, mrongo.

2- Kuhusu uulizaji wako kuhusu adhabu kwa mabalozi na wajumbe, jibu lake linapatikana katika maelezo ya kilma “na” cha Ibara ya 7 katika kitabu, Utangulizi wa Rasimu ya Katiba, na haya ndiyo maandishi yake:

Ama Ibara F, ushahidi unaohusiana na utekelezaji wa kanuni zote za Uislamu unatokana na yale yote ambayo yametajwa hivi punde kwamba kafiri ana wajibu wa kushikamana na misingi na matawi, hivyo basi, ameamrishwa kujisalimisha kwa sheria zote za Uislamu. Hii ni jumla, na inajumuisha Dhimmi na asiyekuwa Dhimmi kutoka miongoni mwa wale wanaoishi chini ya mamlaka ya Uislamu. Kwa hivyo, makafiri wote wanaoingia Dar Al-Islam lazima wakabiliwe na sheria za Uislamu isipokuwa mambo ya´Aqidah, hukmu zinazohusiana na mambo ya´Aqidah na kitendo chochote ambacho Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwaruhusu kufanya iwe makafiri hawa ni Dhimmi, wako chini ya mkataba au wanaotafuta hifadhi. Hata hivyo, mabalozi na mfano wao wametengwa kutokana na hili na hukmu za Uislamu hazitatabikishwa juu yao kwani watapewa kile kinachojulikana kama kinga ya kidiplomasia. Hii ni kwa sababu Ahmed amepokea kutoka kwa Ibn Masoud ambaye amesema:

**جَاءَ ابْنُ النَّوَّاحَةِ وَابْنُ أُثَالٍ، رَسُولاَ مُسَيْلِمَةَ إِلَى النَّبِيِّ ﷺ، فَقَالَ لَهُمَا: أَتَشْهَدَانِ أَنِّي رَسُولُ اللَّهِ؟ قَالاَ: نَشْهَدُ أَنَّ مُسَيْلِمَةَ رَسُولُ اللَّهِ، فَقَالَ النَّبِيُّ ﷺ: آمَنْتُ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ، لَوْ كُنْتُ قَاتِلاً رَسُولاً لَقَتَلْتُكُمَا، قَالَ عَبْدُ اللَّهِ: قَالَ: فَمَضَتِ السُّنَّةُ أَنَّ الرُّسُلَ لاَ تُقْتَلُ**

“Ibn Nawwaha na Ibn Uthal walikuja kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kama wajumbe Musaylama - mrongo - na Mtume wa Mwenyezi Mungu akawaambia: “Je, mnashuhudia kwamba mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu?” Wakasema: “Tunashuhudia kwamba Musaylama ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.” Hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: Mimi ninamuamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake. “Mimi nakupeni usalama kupitia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kama ingekuwa mimi ni mwenye kumuua mjumbe ningekuuweni nyinyi wawili.” Abdullah amesema: dhihirisho la sunna hii ni kwamba wajumbe hawauwawi.” (Imepokewa na Ahmad na kutangazwa kuwa ni Hasan na Al-Haythami). Kwa hivyo, riwaya hii inaashiria kwamba hairuhusiwi kuwauwa wajumbe wa makafiri na wala kuwawekea adhabu (Uqubat). Hata hivyo, hii inatumika pekee kwa wale ambao wana nafasi ya mjumbe kama vile balozi na "Charge d'affaires" na kadhalika. Ama wale ambao wadhifa wa mjumbe hauwahusu kama vile mwakilishi (consul) na Mwambata wa Biashara (Commercial Attaché) na mfano wake, hawatakuwa na kinga yoyote kwa kuwa hawana wadhifa wa mjumbe. Jambo hili linapaswa kuregeshwa kwenye mkataba wa kimataifa kwa sababu ni maelezo ya istilahi ambayo uhalisia wake unapaswa kueleweka kwa kuuangalia mkataba na je ni sehemu ya kuthibisha Manat (uhalisia); kwa maana nyengine, kuthibitisha kama wanachukuliwa kuwa wajumbe au la] **Mwisho wa Nukuu kutoka kwa maelezo kutoka katika kitabu, Rasimu ya Katiba.**

Uharamu wa kutoa adhabu ya kifo na adhabu nyenginezo unatekelezeka kwa balozi wa kudumu, kwa balozi na mjumbe wa muda maadamu uhalisia wa “mjumbe” unawahusu. Hakuna tofauti katika suala la kutotoa adhabu kwa balozi wa kudumu na kwa balozi wa muda, kwani wote wawili ni wajumbe ambao sheria za mjumbe zinawahusu katika suala la adhabu.

Ama sehemu ya mwisho ya swali lako: (Pia, iwapo mmoja wa balozi atafanya jinai au atafanya kitendo kisicho halali zaidi ya mipaka yake kama balozi, je, wote wawili wanahukumiwa na kuadhibiwa ipasavyo na Khilafah? Au mabalozi wa muda na wa kudumu wanatendewa tofauti katika suala hili.)

Hatukueleza kwa undani uhalisia wa adhabu zinazojumuishwa chini ya kinga na zile ambazo hazijumuishwi, bali tutalieleza hili kwa kina katika kanuni za utendaji za vifungu vya katiba tulizoanza nazo, na tunamuomba Mwenyezi Mungu atusaidie katika kuzikamilisha kwa wakati muafaka, Mwenyezi Mungu akipenda.

**Natumai kuwa haya yanatosheleza, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Zaidi na Mwingi Hekima.**

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**6 Safar Al-Khair 1445 H**

**22/8/2023 M**